



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI



**MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE**

**14/12/2021**

**MAHUDHURIO:**

1. Bw.Simeon N. Waryuba - Mwenyekiti
2. Bw. Emmanuel A.Kibona - Katibu
3. Bw.Wilfred Mwita - Mjumbe
4. Bw.Victor Rutonesha - Mjumbe

**WAJUMBE WAKARIBISHWAJI**

1. Bi.Veronica C.Lukanda - Mwanasheria

**SEKRETARIETI**

1. Bw.Selemani Kapinga - Afisa Ugavi msaidizi
2. Bw.Frolence Kyabachubya -Afisa Ugavi msaidizi

**Agenda za Kikao**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Agenda
3. Mwongozo maelekezo ya utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa majengo ya kutolea huduma za dharura(EMD), Wagonjwa mahututi(ICU), Wodi ya magonjwa ya mlipuko(Treatment Centre) na nyumba za watumishi.
4. Kibali cha kuanza ujenzi wa nyumba ya watumishi Hospitali ya Wilaya Tsh.90,000,000/-
5. Kibali cha kuanza ujenzi wa Shule ya sekondari Morotonga kupitia mradi wa SEQUIP TSH 470,000,000/=
6. Kibali cha Kutumia TSH 2,380,000,000/= katika ujenzi wa madarasa 119 ya covid-19 ya Shule za sekondari na Msingi
7. Mengineyo
8. Kufunga Kikao.

**AGENDA NO.1 KUFUNGUA KIKAO**

- Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa 9.30 mchana kwa kuwakaribisha wajumbe katika kikao hicho na kuwalishwa wajumbe kuwa kikao hicho ni cha kawaida katika utekelezaji wa majukumu ya kitengo cha manunuzi.

## **AGENDA NA.2 KUTHIBITISHA AGENDA**

Katibu alifafanua kuwa agenda zipo saba na kuwaomba wajumbe kuafikiana kuwa agenda hizo ndizo ambazo watakazojadiliana. Wajumbe waliridhia agenda zote saba.

### **AGENDA NA 3 MWONGOZO MAELEKEZO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA UJENZI WA MAJENGU YA KUTOLEA HUDUMA ZA DHARURA(EMD), WAGONJWA MAHUTUTI(ICU), WODI YA MAGONJWA YA MLIPUKO(TREATMENT CENTRE) NA NYUMBA ZA WATUMISHI**

Mwenyekiti aliomba Mjumbe katibu atuongoze katika agenda hiyo ya maelekezo ya utekelezaji wa Miradi katika taarifa husika iliyotolewa na kuwawezesha wajumbe kutoa mapendekezo mbalimbali katika utekelezaji wa miradi hiyo kwa kupendekeza

- Kutumia Taasisi za umma katika kazi za ujenzi wa miradi hiyo
- Kutangaza kazi hizo za ujenzi kwa njia ya force account na kufuata sharia Ya manunuzi ya umma.
- Kwa miradi ya ujenzi wa majengo ya EMD & ICU yatahitaji kutumia Wakandarasi watakaoteuliwa wasiokuwa chini ya daraja la 4, Isipokuwa kwa nyumba ya watumishi Hospitali ya Wilaya kupendekeza kutumia njia ya force account.

### **AGENDA NO.4 KIBALI CHA KUANZA UJENZI WA NYUMBA YA WATUMISHI HOSPITALI YA WILAYA TSH.90,000,000/-**

Katibu alieleza uwepo wa uidhinishwaji wa Dokezo na fomu namba mbili (2) ya ujenzi wa nyumba za watumishi Hospitali ya Wilaya lenye thamani ya Tsh.90,000,000/- na wajumbe wa bodi ya zabuni walishauri utaratibu wa manunuzi kwa Kutumia Taasisi Umma katika shughuli za ujenzi uendeleee .

### **AGENDA NO.5 KIBALI CHA KUANZA UJENZI WA SHULE YA SEKONDARI MOROTONGA KUPITIA MRADI WA SEQUIP TSH 470,000,000/=**

Katibu aliwasilisha dokezo na fomu namba mbili juu ya ujenzi wa shule ya sekondari ya morotonga, na imeidhinishwa na mkuu wa idara na mkurugenzi Wajumbe wa kitengo cha manunuzi wanashauri kutumia taasisi za serikali katika ujenzi wa shule ya sekondari Morotonga na kuwanunulia vifaa ili kazi iweze kutekelezwa kwa haraka na makini kupitia mradi wa SEQUIP na kuchukua maamuzi ya kutangaza kazi kwa wazabuni wengine endapo ukosefu wa wazabuni wa taasisi umma watakasekana kwa mfumo wa force account.

### **AGENDA NO.6 KIBALI CHA KUTUMIA TSH 2,380,000,000/= KATIKA UJENZI WA MADARASA 119 YA COVID-19 YA SHULE ZA SEKONDARI NA MSINGI KWA KUTUMIA FORCE ACCOUNT.**

Katibu aliwasilisha dokezo na fomu namba mbili juu ya ujenzi wa madarasa 119 ya covid 19 sekondari na msingi kwa kutumia force account .  
Wajumbe wa bodi ya zabuni walipitisha nakushauri kazi iendelee kwa kufuta taratibu za manunuzi kwa kila hatua.

#### **AGENDA NO.7 MENGINEYO**

Wajumbe walishauri uaandaji wa tangazo la kazi ya ujenzi wa nyumba ya watumishi ya hospitali ya wilaya na Kazi ya ujenzi wa shule ya sekondari morotonga kuweza kuwasilishwa katika bodi ya zabuni  
Mjumbe walishauri kuwa unahitajika muda wa kutosha ili kuweze kutekeleza kazi kwa wakati na ubora.


#### **AGENDA NO.8 KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa michango yao na alifunga kikao mnamo saa 11.20 jioni.  
Umesainiwa leo tarehe.....29/12/2021.....



.....

Saini  
KATIBU



.....

Saini  
MWENYEKITI